**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO (CMT)**

**KWENDA KWA:** WAKUU WA IDARA NA VITENGO

**KUTOKA KWA:** AFISA UTUMISHI NA UTAWALA (W)

**Kumb Na: AJ.81/177/321/104**

**YAH: MAMBO YA KUFANYIA KAZI KUFUATIA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 26/01/2022.**

**MAHUDHURIO:**

**A: WATAALAMU WALIOHUDHURIA: KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 26/01/2022.**

1. Bw. Denisi kitali -Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Bw. Sud S. Khassimu -Kaimu Afisa Utumishi(W)
3. DR. Elizabeth Oming'o -Mganga Mkuu (W)
4. Bi. Rehema Isaay - Mwekahazina (W)
5. Bw. Tumainiel Kamnde -Afisa Manunuzi (W)
6. Bw. Rudrick Charles -Afisa Mipango (W)
7. Bw. Anthony Nyange -Afisa Maendeleo ya Jamii(W)
8. Bw.Mfaume S.Jeta -Afisa TEHAMA
9. Bw.Bwenda I. Bainga -AfisaKilimo, Umwagiliaji(W)
10. Bw. Swalehe Njoma -Mwanasheria (W)
11. Eng.kassim Mponda -Kaimu Mhandisi Ujenzi(W)
12. Bw.Laban Kitule -Kaimu Afisa Mazingira
13. Bw.Damas Kimaro -Kaimu Afisa Elimu Msingi
14. Bw. Jamal Saidi -Mratibu TASAF (W)
15. Bw. Hamadi Mgaluli -Kaimu Afisa Nyuki (W)
16. Bw.Justus Lugome - Kaimu Afisa Elimu Sekondari

**B. WASIO HUDHURIA KWA TAARIFA.**

1. Bw. Mohamed I. Mavura -Mkurugenzi Mtendaji(W)
2. Bw. Mkoyongi J. Manyama -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi

**C. SEKRETARIET.**

1. Bw. Mao Kasanga -Mwandishi wa Vikao
2. Bi. Raya Mlawa -Mwandishi wa Vikao

**AGENDA NA. 01: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alikaribisha Wajumbe kikaoni, alieleza kuwa kikao cha Menejimenti cha Kila jumatano ya wiki hivyo aliomba wajumbe kuwa makini katika kujadili taarifa zinazowasilishwa.
Ilielezwa kuwa Leo tarehe 26/01/2022 kutakuwa na kikao cha Chama cha Mapinduzi kujadili utekelezaji wa ilani ya Chama, hivyo Wakuu Wote wa Idara na vitengo wametakiwa kuwepo kwenye kikao hicho na kujibu hoja za idara zao ambazo zitawasilishwa.
Baada ya kusema hayo alifungua kikao saa 08:28 Asubuhi.

**AGENDA NA. 02: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO.**
Jumla ya agenda Tisa (9) ziliwasilishwa kikaoni ili zijadiliwe nazo ni;

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa tarehe 26/01/2021.
4. Yatokanayo na kikao cha CMT cha tarehe 26/01/2021
5. Taarifa ya Mapato ya Wiki kuanzia tarehe 17/01/2022 Hadi 23/01/2022
6. Taarifa ya DEFAULTER's
7. Taarifa ya Mapokezi ya kiasi cha fedha **Tshs. 90,000,000.00** kwaajili ya Ujenzi wa Nyumba za 3/1 mbili za Watumishi kituo cha Afya Nyamatanga
8. Taarifa za Utekelezaji wa Kazi za Idara.
9. Kufunga kikao.

Baada ya agenda hizo kupitiwa Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia agenda zote Tisa (9) Kujadiliwa.

**AGENDA NA 07: TAARIFA YA MAPOKEZI YA KIASI CHA FEDHA TSHS. 90,000,000.00 KWAAJILI YA UJENZI WA NYUMBA ZA 3/1 MBILI ZA WATUMISHI KITUO CHA AFYA NYAMATANGA.**

Kwa idhini ya Mwenyekiti Mweka hazina aliwasilisha taarifa ya Mapokezi ya fedha kama ifuatavyo;-
Ilielezwa kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha fedha **Tshs. 90,000,000.00** kutoka Serikali kuu ikiwa ni Fedha za UVIKO-19, ilielezwa kuwa fedha hizo zimeingia tarehe , 20/01/2022 siku ya Alhamisi.

Ilielezwa kuwa fedha hizo ni kwaajili ya Ujenzi wa nyumba za Watumishi 3/1 Kituo cha Afya Nyamatanga Kata ya Ruaruke.
Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa Menejimenti ilisisitiza Maandalizi ya awali yafanyike, barua ya taarifa ya mapokezi ya fedha ipelekwe Kwa mtendaji Kata pamoja na Mhe. Diwani ili wananchi wapatiwe taarifa.
Menejimenti ilisisitiza maandalizi ya Ujenzi yaanze kufanyika mapema ili kumaliza ndani ya muda.
Baada ya Mjadala huo Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia na kupitisha

**AGENDA NA 10: KUFUNGA KIKAO.**
Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa miachango yao na kusisitiza yaliyoagizwa yakafanyiwe kazi. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 04:00 Asubuhi.

*MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;*

| | |
|---|---|
| [signature] | [signature] |
| **SAINI YA MWENYEKITI** | **SAINI YA KATIBU** |
| DENIS KITALI | SUDI S.K |
| **JINA LA MWENYEKITI** | **JINA LA KATIBU** |
| 26/01/2022 | 26/01/2022 |
| **TAREHE** | **TAREHE** |